FASIHI SIMULIZI

UTABIRI WA KCSE

Maswali ya Marudio Matarajiwa Katika Mtihani Mkuu wa KCSE.

MARUDIO KATIKA SEHEMU YA FASIHI SIMULIZI.

SERIES 2

Ukihitaji majibu,
Pigia Bw. Isaboke 0746 222 000
AU *0742 999 000*

MWALIMU CONSULTANCY

USHAIRI SIMULIZI.

1) Eleza maana ya ushairi simulizi.

2) Fafanua sifa zozote nane za ushairi simulizi.

3) Ushairi simulizi huainishwa kwa vigezo kadhaa. vitaje

4) Huku ukitoa mifano, eleza dhima zozote kumi za ushairi simulizi.

5) Ainisha vipera vikuu vya ushairi imulizi.

6) Fafanua sifa saba za Maghani

7) Taja aina mbili kuu za maghani.

8) Vipera vya maigizo ni vifuatavyo:.

9) Eleza maana ya majigambo/vivugo.

10) Eleza sifa zozote tano za majigambo

11) Huku ukitoa mifano, jadili hasara za majigambo katika jamii.

12) Fafanua mbinu zozote kumi zinazoweza kufanikisha uwasilishaji wa majigambo.

13) Fafanua maana ya Maghani ya masimulizi.

14) Ainisha Vipera vya maghani ya masimulizi

15) Fafanua sifa za Tendi katika ushairi simulizi

16) Eleza maana ya Ngonjera.

17) Eleza maana ya nyimbo.

18) Eleza sifa za kimuundo katika kipera cha nyimbo.

19) Eleza Utendaji wa nyimbo katika fasihi simulizi

20) Fafanua sifa za kishairi za Nyimbo

21) Fafanua Umuhimu wa upigaji makofi katika uwasilishaji wa wimbo.

22) Taja vigezo vinavyozingatiwa katika kuainishwa Nyimbo

23) Eleza maana ya Nyiso.

24) fafanua sifa na umuhimu wa nyiso

25) Eleza maana ya Sifo / tukuzo.

26) Fafanua sifa za sifo katika jamii

27) Jadili umuhimu wa sifo au tukuzo katika jamii

28) Mbolezi / tahalili ni nini?

29) pambanua sifa za mbolezi katika jamii

30) Jadili Umuhimu wa mbolezi.

0746 222 000

UTANGULIZI WA FASIHI

1) Eleza kwa tafsili maana ya fasihi.

2) Ainisha tanzu mbili kuu za fasihi.

3) Tofautisha kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

4) Fafanua Uhusiano / ubia uliopo baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

5) Huku ukitoa mifano kem kem, eleza dhima zozote tano za fasihi simulizi.

6) Fafanua Maana ya fasihi simulizi.

7) Taja Vipengele muhimu katika uwasilishaji wa fasihi simulizi.

8) Orodhesha vipera vikuu vya fasihi simulizi

9) Taja na ufafanue sifa bainifu za fasihi simulizi.

MASIMULIZI / HADITHI

1) Eleza kwa tafsili maana ya ngano/ hadithi.
2) Fafanua Vipengele muhimu katika uchanganuzi wa hadithi.
3) Taja na ueleze aina zozote tano za ngano/hadithi.
4) Fafanua sifa zozote tano za hadithi.
5) Jadili Umuhimu wa utangulizi maalum katika utambaji wa hadithi.
6) Eleza Umuhimu wa kiishio maalumu katika utambaji wa hadithi.
7) Ni kwa nini ngano zilitambwa usiku?
8) Eleza Umuhimu wa nyimbo katika utambaji wa ngano
9) Jadili Sifa bainifu za mtambaji bora
10) Fafanua majukumu ya ngano au hadithi.
11) Eleza maana Visasili.
12) Jadili dhima ya visasili katika jamii.
13) Eleza kwa fasilili maana hadithi ya kiayari.
14) Jadili sifa mbalimbali za hadithi ya kiayari.
15) Fafanua Umuhimu wa hekaya katika jamii
16) Hurafa ni nini?
17) Eleza Sababu nne za fanani au mtambaji kutumia wahusika wanyama katika hurafa:
18) Eleza Sifa sita za hadithi ya hurafa

0746 222 000

19)Ngano za mazimwi ni hadithi za aina gani?

20)Ainisha sifa za ngano za mazimwi.

MAIGIZO

1) Eleza maana ya maigizo katika fasihi simulizi.

2) Fafanua sifa za Maigizo katika jamii

3) Huku ukitoa mifano, ainisha aina mbili kuu za maigizo.

4) Pambanua sifa za Maigizo ya kawaida

5) Taja vipera vikuu vya maigizo.

6) Eleza maana ya Vichekesho.

7) Vichekesho huwa na sifa kadhaa. jadili

8) Eleza Umuhimu wa vichekesho.

9) Eleza maana ya miviga/mivigha.

10) Fafanua sifa zozote nane za miviga.

MAZUNGUMZO

1) Mazungumzo ni nini katika fashihi simulizi?

2) Ni nini maana ya ulumbi.

3) Taja tanzu mbili kuu za ulumbi

4) Eleza sifa zozote kumi za ulumbi au mlumbi.

5) Eleza umuhimu wa ulumbi kama fani ya mazungumzo katika jamii.

6) Huku ukitoa mifano, bainisha sifa nne za malumbano ya utani.

7) Fafanua majukumu matano ya malumbano ya utani katika jamii.

8) Fafanua changamoto mbalimbali zinazokabili malumbano ya utani

9) Eleza maana ya Mawaidha.

10) Huku ukitoa mifano, bainisha sifa nne za Mawaidha

11) Ni mambo yepi ambayo huuhusisha katika uwasilishaji wa mawaidha?

12) Taja vigezo vinavyozingatiwa katika kueleza Mawaidha

13) Eleza dhima zozote saba za mawaidha katika fasihi simulizi.

14) Fafanua maana ya maapizo.

15) Eleza sifa zozote tano za maapizo.

0746 222 000

16) Eleza umuhimu wa maapizo katika jamii.

17) Eleza maana ya Soga.

18) Fafanua sifa za soga katika fasihi simulizi

19) Jadili umuhimu wa soga

SEMI.

1) Eleza kwa tafsili maana ya semi

2) Eleza sifa nane za Semi katika fasihi simulizi

3) Ainisha mifano minane ya tanzu fupi katika fasihi simulizi.

4) Eleza maana ya methali.

5) Huku ukita mifano, eleza nduni/sifa zozote tano za methali.

6) Huku ukitoa mifano maridhawa, eleza jinsi fani/mtindo/ matumizi ya lugha yanavyodhihirika katika methali. Eleza muundo wa methali kwa mujibu wa tamathali za lugha mbalimbali.

7) Jadili dhana ya uianishaji/ vigezo vinavyotumika katika uainishaji wa methali.

8) Eleza uamilifu /majukumu mbalimbali ya methali katika jamii

9) Eleza kwa tafsili maana ya vitendawili.

10) Huku ukitoa mifano, ainisha/eleza aina zozote nne za vitendawili.

11) Fafanua sifa bainifu zozote tano za vitendawili

12) Huku ukitoa mifano, eleza dhima zozote kumi za vitendawili katika jamii.

13) Fafanua Mtindo au fani mbalimbali katika vitendawili.

14) Eleza uwiano na tofauti baina ya vitendwili na methali.

15) Eleza maana ya Mafumbo.

16) Fafanua sifa saba za Mafumbo

17) Jadili Umuhimu wa mafumbo.

18) Fafanua maana ya nahau.

19) Jadili sifa tano za Nahau

20)taja mitindo na muundo mbalimbali wa nahau

21) Fafanua Umuhimu wa nahau.

22) Fafanua maana ya Misemo.

23) Taja sifa zote saba za Misemo

24) Eleza Umuhimu wa misemo katika jamii ya sasa.

0746 222 000

25) Tanakali za sauti ni nini ?

26) Fafanua sifa zozote za tanakali za sauti

27) Jadili Umuhimu wa tanakali za sauti.

28) Eleza maana ya vitanza ndimi.

29) Fafanua sifa zozote tano za vitanza ndimi.

30) Eleza dhima zozote kumi za vitanza ndimi.

UTAFITI WA FASIHI SIMULIZI

1) Eleza maana ya utafiti.

2) Fafanua hatua muhimu/ vipengele vya kimsingi katika utafiti wa fasihi simulizi.

3) Eleza matatizo au vizingiti vyovyote kumi vinavyoweza kumkabili mtafiti wa fasihi simulizi.

4) Fafanua mikakati ya kuendeleza fasihi simulizi.

5) Jadili Vikwazo vinavyotinga ukuaji wa fasihi simulizi.

6) Jadili Umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi.

7) Eleza Umuhimu wa utafiti wa fasihi simulizi.

8) Taja Mambo yanayosababisha kubadilika kwa fasihi simulizi.

9) Jadili Mchango wa fasihi simulizi kwa fasihi andishi.

10)jadili Uhifadhi wa kazi ya fasihi

11) Jadili Athari za mbinu mbalimbali za uhifadhi za fasihi simulizi.

12) Fafanua Mbinu zozote sita za kuhifadhi na kukusanya data.

0746 222 000

MASWALI MENGINE YA FASIHI SIMULIZI

1. *Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali*

Hapo zamani za kale, Nyani na Mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya Mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile Mamba alikuwa mvuvi msahuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea Mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.

Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri Zaidi wakati Mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na Mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa Ng'ombe. Wakatenda mengi pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete.

Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na Mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya Mamba ya uvuvi ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara Mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya Mamba. Hali hii ilitishia kuutia ufa urafiki kati ya Mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona. Nyani au watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri aalivyojaribu kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyoendelea kumshauri, "Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo? Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye anajiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama? Hata karafuu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta. "Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa Nyani alikuwa mla naye tu.

Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwake akihesabu nyota, wazo lilimjia. Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi ilia pate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejinamia kwa jitimai. Alisema, "Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi," Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi Mamba kwamba wangeandamana pamoja. Kwa vile

0746 222 000

Nyani hangeweza kutembea majini, ilibidi abebwe na Mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo, Mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa Mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, Mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. "Rafiki yangu, nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati, kumbe uzuri wako wa mkakasi? Mimi na wanangu tumetafunwa na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo lisilo budi hutendwa."

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wenyewe ujikabidhi kwa Mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia Mamba,"Ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Unajua tena sisi Nyani, Tumbili na Kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo, nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya wanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo."

Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile Mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amletee mioyo.

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumchelewesha Nyani. Matumbo yalimnguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akongoja, akangoja... wiki, mwezi, mwaka... Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari. Huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na Mamba. ***Hadithi yangu inaishia hapo.***

a) Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. **(alama 2)**

b) Tambua mbinu **sita** kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. **(alama 6)**

c) Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo **matano** muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. **(alama 5)**

d) Fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii. **(alama 3)**

e) Kwa kutoa hoja **nne** jadili umuhimu wa maneno yaliyokolezwa rangi katika utambaji wa ngano kama hizi. **(alama 4)**

0746 222 000

2. ***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali***

Ewe Mainga wa Ndumi Siwe uloambia akina mama Siku tulopiga foleni Chakula cha msaada kupata

Turudishe vifaranga kwenye miji Wageuke vijusi tena

Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita Matusi ukitema

Chumvi na sukari kuturushia ja samadi? Uhitaji wetu ukatutuma

Kuokota vihela uloturushia Ukatununua, kura ukapata? Sasa miaka mitano imetimia Waja tulaghai tena

Mainga wa Ndumi huna lolote safari hii Ubunge umekudondoka ukitazama Wanyonge tumeamua

Kwingine kujaribu.

a) Eleza aina ya kipera hiki. **(alama 2)**

b) Huku ukitoa mifano, tambua mbinu za lugha nne zilizotumiwa katika utungo huu**.(alama 8)**

c) Tambua nafsineni katika utungo huu. **(alama 2)**

d) Fafanua toni ya utengo huu. **(alama 2)**

e) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. **(alama 6)**

3. ***Soma hadithi hii kisha ujibu maswali***

Ilikuwa alfajiri yenye baridi. Umande ulitapakaa kote. Ukungu ulitanda hivi kwamba hungeweza kumuona mtu alikuwa hatua chache mbele yako.Ndovu alipoamka, alikuta fisi mlangoni pake. Fisi alikuwa amemlimia ndovu shamba lake, lakini alikuwa hajalipwa ujira wake.

Kila alipomwendea ndovu kwa ajili ya malipo yake, fisi alitiliwa huku na kutolewa kule.”Leo ni leo”,fisi alimwambia ndovu.”Nimevumilia vya kutosha. Kila siku ninapokuja kuchukua pesa zangu, hukosi hadithi mpya ya kunisimulia. Leo sitoki hapa bila pesa zangu!”

Fisi alipomaliza kumwaga joto lake, ndovu alimwambia: “Sikiliza fisi. Mimi nimeheshimika kote kijijini. Naona haja yako ni kunivunjia heshima –mbele ya familia yangu na wanakijiji kwa jumla. Sikulipi pesa zako, mpaka ujifunze kuwaheshimu wazee. Nakuamuru uondoke hapa mara moja, kabla sijakasirika! Nataka uende popote, unapofikiria kwamba unaweza kupata msaada. Ukienda kwa chifu, usisahau kwamba tunakunywa na yeye. Ukienda polisi, mkuu wa kituo amejaa tele mfukoni mwangu. Ukienda mahakamani, hakimu tulisoma darasa moja. Popote uendapo, hakuna yeyote atakayekusikiliza”

“Zaidi ya hayo, hakuna yeyote atakayekuamini.Mimi naitwa Bwana pesa.Kwangu umeota mpesapesa na kustawi. Nani ataamini kwamba naweza kushindwa kulipa vijisenti vichache ninavyodaiwa na fisi?”

Fisi alisikiliza kwa makini majitapo ya ndovu. Aliamua kumpasulia ndovu mbarika: "Bwana ndovu najua kuwa wewe una nguvu na uwezo mkubwa wa kifedha.Lakini hayo yote mimi hayanihusu ni yako na familia yako. Sitakuruhusu unidhulumu kilicho haki yangu. Usiutumie uwezo uliopewa na Muumba kuwaonea na kuwanyanyasa maskini wasio mbele wala nyuma" alimaliza usemi wake na kuondoka huku machozi yakimdondoka.

Fisi alipofika nyumbani, aliwasimulia fisi wanyonge wenzake yaliyomsibu.Fisi walikusanyika na kulizingira boma la ndovu huku wakisema: "Tunataka haki itekelezwe! Dhuluma lazima ikome! Unyanyasaji lazima ukome!" Ndovu aliposikia kelele langoni mwake, alipiga simu kwenye kituo cha polisi.

Mara, kikosi cha polisi wa kupambana na ghasi kiliwasili. Fisi walipigwa mijeledi na kuezekwa marungu. Waliojifanya mabingwa walipigwa risasi. Fisi waliosalia walikimbilia makwao, huku wakichechemea kwa maumivu. Mpaka wa leo fisi wangali wanatembea kwa kuchechemea.

Maswali

a) Usimulizi huu ni wa aina gani? Toa sababu. **(alama 4)**

b) Eleza mtindo wa lugha uliotumika katika hadithi hii. **(alama 4)**

c) Eleza sifa za ndovu katika hadith hii. **alama 5)**

d) Fafanua jinsi kisa hiki kinavyo dhihirisha methali: 'Mwenye nguvu mpishe' **(alama 4)**

e) Je, hadithi zina umuhimu gani katika jamii? **(alama 3)**

4. ***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.***

Hapo zamani paliondokea kuku na mwewe. Ndege hawa walikuwa masahibu wa kufa na kuzikana. Waliishi pamoja kwa miaka na mikaka. Walishirikiana na kusaidiana kwa lolote lilipotokea, la majonzi na furaha.

Walishirikiana katika kazi zote zilizowahusu. Kila mmoja wao alikuwa na bidii ya mchwa walipofanya kazi. Waligawanya kazi mbalimbali na kuzifanya bega kwa bega. Kazi ya mwewe ilikuwa kutafuta chakula chao cha kila siku naye kuku alikuwa na wajibu wa kuwalinda watoto wao. Alihitajika kuwapa chakula cha kutosha na kuhakikisha walitulia. Kuku pia alihitajika kuwaamsha wengine kulipokucha.

Siku moja, kuku na mwewe walialikwa katika karamu fulani na ndege wenzao. Walitarajia kwenda karamuni pamoja na watoto wao. Mwewe aliandaa wanawe na kuhakikisha kuwa walikuwa tayari kwa karamu hiyo kubwa. Katika harakati za maandalizi, Kuku naye

0746 222 000

aligundua kuwa vifaranga wake walikuwa na kucha ndefu zilizoonekana mbaya. Aliamua kumwomba mwewe wembe, “tafadhali nipe wembe nikatie kucha wanangu. “Haya chukua. Hakikisha umeurejesha, la sivyo..”

Alipoupokea wembe, alimshukuru rafikiye kisha akaanza kukata kucha za vifaranga wake. Alikata kucha za vifaranga watatu vizuri lakini alipokuwa akishughulikia wa nne, wembe ulimponyoka na kuanguka. Alijisemea kwa masikitiko, “Ole wangu mie, wembe wa mwewe nitaupata wapi? Mwewe alipomaliza kujitayarisha alimwita kuku waende karamuni.

Kuku aliyekuwa na wasiwasi alikataa kwenda huku akisingizia maumivu mwilini, mwewe aliwachukua wanawe na kujiendea karamuni.

Baada ya mwewe kuondoka, kuku alirudi nje na kuanza kuchakurachakura chini mahali alikuwa akiwakatia vifaranga kucha. Alitafuta hadi machweo bila kufua dafu. Mwenye wembe aliporudi alimuuliza,

“kulikoni ndugu kuku?”

“Ah, eh, wembe, wajua wembe wako u u u...” “wembe umefanya nini? Isije kuwa umeupoteza!” “kwa kweli ndio ume...potea”

“Aka! Hujui wewe huo wembe ni mmoja kama roho. Lazima nitwae fidia. Nitawala vifaranga wako mmoja mmoja hadi uniregeshee wembe wangu.”

Tangu siku hiyo kuku huchakurachakura chini akitafuta wembe wa mwewe naye mwewe huruka juu akiwasaka vifaranga vya kuku.

a) Ainisha kipera hiki. Toa sababu. **(alama 2)**

b) Eleza sifa za kipera umetambua hapo juu. **(alama 5)**

c) Fafanua majukumu ya kipera hiki katika jamii. **(alama 5)**

d) Fafanua mtindo katika kifungu hiki. **(alama 4)**

e) Eleza sifa nne za fanani bora. **(alama 4)**

0746 222 000

5. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali***

Heri ujue mapema Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu,humea kwa kina mamaku. Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah!kisu cha ngariba ni kikali ajabu. Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasotabiri, Ama tukwite njeku.
Mpwangu kumbuka hili, Wananume wa mlango wetu Si waoga kwa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

Maswali

(a) Taja na uthibitishe shughuli zozote za jamii ya wimbo huu. (**alama 4**)

(b) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? (**alama 2**)

(c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha. (**alama 2**)

(d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume .Thibitisha kauli hii. (**alama 2)**

(e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii. (**alama 6**)

(f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri ,zina ubaya wake.Thibitisha kauli hii . (**alama 4**)

0746 222 000

6. T***umia kifungu kifuatacho kujibu maswali yanayofuata***

a) Nyumbani mwetu mna papai lilioiva lakini siwezi kulichuma – ndugu wa kiume asimuoe nduguye wa kike.

i) Bainisha kipera kinachorejelewa **(Al 1).**

ii) Andika shughuli moja ya Kijamii na moja ya Kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utingo huu. **(Al 2)**

iii) Eleza dhima nne za kipera kinachorejelewa katika jamii yako. **(Al 4)**

iv) Wewe ni mwasilishaji wa kipera hiki jukwani. Eleza mambo manne ambayo utazingatia katika uwasilishaji wako. **(Al 4)**

b) Umepewa jukumu la kukusanya data kuhusu michezo ya watoto ukitumia hojaji.

i) Eleza manufaa **manne** ya kutumia mbinu hii. **(ala. 4)**

ii) Eleza changamoto **nne** za kutumia mbinu hii. **(ala. 4)**

c) Fafanua majukumu yoyote manne ya nyimbo katika jamii. **(Al 4)**

7. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Ndimi Chesirwo, kijana barubaru,
Ndume na gwiji, la ukoo mtukufu, Najivunia umahiri, kusakata kandanda.

Tazama umbo langu, guu mithili ya jokovu, Kifua cha miraba, weusi wa kijungu, Wenzangu wanienzi, na hata kuduwaa.

Misuli ni tinginya, Kijijini nasifika, Wazee kunienzi, Mabinti kunikabidhi.

Maswali

(a) Tambua utungo huu na uthibitishe jibu lako. **(alama 2)**

(b) Kwa kurejelea hoja zozote nane, jadili sifa za utungo uliotambua katika (a) **(alama 8)**

(c) (i) Eleza maana ya maghani. **(alama 1)**

(ii) Taja na ueleze tofauti za aina mbili za maghani. **(alama 4)**

(d) Eleza jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi. **(alama 5)**

0746 222 000

8. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:***

Wanangu, mwanadamu lazima awe na malengo ya mambo anayohitaji kuyatekeleza siku za maisha yake duniani kabla ya maisha ya baada ya kifo. Ni lazima akumbuke kuwa si vyema akubali kufa kama kwamba hakuwahi kuishi duniani. Yaani, haifai kwa mtu yeyote kuondoka duniani na kuelekea peponi kuishi kwa starehe ama ahera kwa wale wanaokufa kabisa, bila kuacha lolote lenye mashiko duniani. Lazima kuhakikisha kwamba kuna bora, japo moja, ambalo waliosalia duniani watakukumbuka kwalo. Japo kiduchu tu. Ukiwa mwimbaji imba lau ubeti mmoja tu ukasikizwe wakati utakapokuwa umepumzika. Ukiwa kiongozi jenga daraja japo moja na kulizindua wewe. Mwili wako utakuwa umeondoka ila nafsi yako itasalia duniani kwa jina lako.

Ukiwa na mkono wa kuandika andika japo ubeti mmoja wa shairi. Kumbusha watu kuhusu umuhimu wa maisha na kuwaeleza kutenda mema kabla hawajaisha. Andika hata aya tatu za hadithi. Jihusishe katika mashindano maarufu japo ujue kuwa wahariri wataiangalia kazi yako na kusema, "Uchafu mtupu! Huyu hana talanta. Ameharibu wakati wake tu katika shindano hili la jumuia nzima. Sisi tunasaka talanta! Huyu limbukeni anatuletea hapa 'viswahili' gani hivi visivyo na mkia wala kichwa hali mwenyewe si Mswahili? Potelea jalalani! Huenda hata wakati mwingine kazi yako isisomwe ila wewe andika tu. Andika tena na tena. Andika.Andika usihofu. Bora tu usife kama hukuwahi kuishi.Zingatieni wosia wangu huu wanangu.

(*Kutoka Riwaya: Hawakuziki Mama- Meja S. Bukachi*)

(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi. **(Alama 2)**

(b) Fafanua vipengele kumi vya kimtindo ambavyo fanani ametumia katika uwasilishaji wake. **(alama 10)**

(c) Eleza umuhimu wa kipera hiki katika jamii. **(alama 3)**

(d) Wewe ni kati ya wanaopewa kipera hiki. Fafanua mambo matano ambayo wewe na wenzako mnaweza kufanya wakati wa kutolewa. **(alama 5)**

9. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.***

Mimi ni morani Nguli aliyekamilika
Nishatoka kumrarua simba dume Kwa hii mikono miwili
Mimi ni shujaa asiyekanyanga kwa woga Wala kubabaika

0746 222 000

Simba mwenyewe ameungama Mkuki wangu ni shahidi.

Mimi ni Jabali mtetemesha ardhi Azma yangu hairudi nyuma Nguvu zangu hazimithiliki

Sina mzaha wala dhihaka Mimi ni jasiri

Ngao ndio hii hapa mkononi ni Fumo nilirithi Kujikinga na kulinda hadhi yangu

Yu wapi mwingine shujaa?

Mawali.

a) (i)Andika aina ya sifo hii. **(alama 1)**

(ii) Toa sababu **nne** kuthibitisha jibu lako la (i) hapo juu. **alama 2)**

(iii) Tambua mbinu **mbili** la lugha zilizotumiwa katika utungo huu**. (alama 2)**

b) (i) Eleza sifa **saba** za utungo huu. **(alama 7)**

(ii) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii nyingi. Fafanua kwa hoja **nane** sababuza hali hii. **(alama 8)**

10. ***Soma maagizo yafuatayo kisha ujibu maswali***

(Alfajiri kuu. Vijana wanazunguka kinu, vifua wazi. Nyusoni wamepakwa masizi na aina ya tope jeupe. Wako katikati yam situ. Mzee Jando ameketi kwenye namna yam to wa nyasi.)

Mzee Jando: (Akiwahiza) haraka! Ongezeni kasi! Zunguka! Haya imbeni, barobaro! Vijana: jua lachomoza!

Muda umefika wa mbegu kuatika! Ichipuke na kuzalisha matunda!

Ni leo, ni sasa! Mzee Jando: haya ketini sasa

Vijana: (Vijana wanaketi katika mistari huku wameshikana mikono mabegani) Mzee Jando: tulisema mume nini?

Vijana: (kwa pamoja na kwa sauti ya dhati) Mume ni kazi

Sio ubazazi Ale jasho lake!

Mzee Jando: Sawa kabisa, je mume ni nani? Vijana: Ni mlinzi wa jamii

Ni mfano mwema wa jitihada Apambane na adui

Atende wajibu na maadili Mzee Jando: Jambo linalovunja umoja!

Vijana: Likumbatiwe na kufunzwa hata watoto wachanga! Mzee Jando: Haya, semeni wenyewe leo!

Vijana: Leo tumkomaa, si watoto tena

Tumetimia barobaro kamili Sisi ni stadi

0746 222 000

Sisi ni wapevu!

Tayari kwa majukumu ya kujenga jamii Sisi ni tegemeo la umma

Sisi ndio chimbuko la wema

Maadili na upendo

Mzee Jando: Nakubali mko tayari. Haya tuendelee na ada zetu zingine. Kijembe kukidhihaki!

Vijana: (Wanasimama kijasiri na kurindimisha sauti) Tuko tayari kuingia utuuzima!

a) Bainisha kipera cha maigizo kinachorelelewa. Thibitisha jibu lako kwa mifano mine.
(al 5)

b) Fafanua matarajio sita ya utuuzima kwa mujibu wa maigizo haya**. (al 6)**

c) Eleza mbinu nne za sanaa ambazo waigizaji wamezitumia katika kuwasilisha maigizo haya**.(al 4)**

d) Unanuia kukusanya data kuhusu kupera hiki, fafanua mbinu sita utakazotumia kukusanyia data huku ukionyesha sababu za utenzi wako. **(al 5)**

11. (a)" **Mwanangu *nakuomba uzingatie uadilifu maishani uongofu ni nuru ya mustakabali wa kila mtu…***"

i) Tambua kipera na utanzu wa tungo hili **(al. 2)**

ii) Kwa kutumia hoja **mbili** eleza muundo wa kipera hiki **(al. 2)**

iii) Fafanua sifa **nane** za kipera hiki **(al.8**

(b) Eleza vikwazo **vinane** vy a ukuaji wa fasihi simulizi. **(al.8)**

12. Dunia hadaa,ulimwengu shujaa.Mnachohitaji mlipofikia, ni ujasiri wa simba kuyakabili maisha.Adabu na bidii yenu leo, ni miche itakayozaa matunda, matunda matamu ya maisha mema kesho.Sitaki muziandame nyendo potovu . Mtakuwa mnajiponza wenyewe
; na hilo litakuwa sawa na kuutumbukiza mustakabali wenu kwenye shimo lenye kina kirefu na giza totoro.Jueni ujana ni moshi na ukienda haurudi.

a) i) Tambua kipera hiki na utoe ithibati. **(Alama 2)**

ii) Ni sifa zipi za kipera hiki zilizojitokeza hapom juu. Eleza kikamilifu **(alama 5)**

b) Misimu hutumia mbinu anuwai katika uundaji wake. Taja tano na utolee mifano mwafaka..
(Alama 5)

c) Eleza mbinu ambazo ungetumia kufanikisha kipera hiki. **(Alama 8)**

0746 222 000

13. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.***

Asiyemjua mjua alionwe atamjua Namjuza kwa sifa zake alizokuwa nazo Alisimika ufalme uliosifiwa

Akawa shujaa asiyetishwa

(a) Tambua kipera hiki **(alama 1)**

(b) Fafanua sifa tano za kipera hiki **(alama 5)**

(c) Tambua aina ya miviga katika jamii ya kisasa **(alama 3)**

(d) Fafanua njia za kuimarisha fasihi simulizi katika ulimwengu wa kisasa. **(alama 5)**

(e) Kwa kurejelea vigezo vitatu onyesha umuhimu wa fani katika kufanikisha usimulizi wa hadithi za fasihi simulizi. **(alama 6)**

14. "Magwiji wa uwanda mpana wa tamaduni za Kiafrika: wazee walioila chumvi wakabobea katika falsafa za turathi zetu, maghuluma wenye misuli tinginya na vifua vya mfumbata vinavyostahimili hujuma za kila nui na malaika wa kike uliosheheni mizinga na chemichemi ya urembo, nawasabahi. Wa zamani waliamba kuwa mwacha mila ni mtuma. Turathi zetu ni uhai. Turathi zetu ni msingi wa ubinadamu wetu. Turathi zetu zinabeba mustakabali wetu. Tuzienzi kama tuenzivyo asali."

a) (i) Tambua kipera cha utanzu wa mazungumzo kinachohusishwa na kifungu hiki.**(alama 1)**

(ii) Thibitisha jibu lako katika (i) kwa mifano yoyote **mitatu**. **(alama 3)**

b) Iwapo umehudhuria utendaji wa kipera hiki nyanjani eleza sifa **tano** za mtendaji utakazoziona zisizojitokeza kwenye kifungu. **(alama 5)**

c) Taja na kueleza miktadha **minne** ambamo kipera hiki kinaweza kutumiwa katika jamii ya kisasa. **(alama 4)**

d) Andika sifa zozote **nne** za jamii ya nafsi neni katika utungo huu. **(alama 4)**

e) Eleza njia **tatu** za ukusanyaji wa data unazoweza kutumia kukusanya data kuhusu kipera hiki**. (alama 3)**

15. a) Wewe ni mwigizaji wa michezo ya jukwaani. Eleza mambo sita ambayo utazingatia ili kufanikisha uigizaji wako. **(alama 6)**

b) Mbinu ya uigaji sauti ina umuhimu gani katika fasihi simulizi: **(alama 4)**

0746 222 000

16. ***Soma utungo ufuatayo kisha ujibu maswali.*** **(alama 10)**

Mwananguuu , ni wewe kweli !

ndimi niliyekupa uhai mwana unoringia, Anokufanya upite ukinitemea mate,

Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika, Miungu na waone uchungu wangu,

Radhi zao wasiwahi kukupa Laana wakumiminie,

Uje kuzaliwa mara mia na wanao,

Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao, Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,

Wakazamwanao wasikuuguze katika utu uzimawake ***(kutoka – Fani ya Fasihi Simulizi)***

i) Tambua kipera hiki cha Fasihi simulizi **(alama 1)**

ii) Eleza sifa zozote nne za kipera hiki cha Fasihi Simulizi **(alama 4)**

iii) Eleza kwa kutoa ithibati jinsia ya nafsineni? **(alama 1)**

iv) Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii. **(alama 4)**

17. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Hawa wanifuatao wananicha, kwa ukoo wangu mtukufu kawa jadi yenye majagina wa mioyo na vitendo wananicha,

Kwa kuwa wa kwanza kijijini kuvishwa taji

kwa mabuku kubukua

kwa kuwa jogoo wa kwanza kuwika kwenye anga za ilimu idhini nikakabidhiwa,

ya tafiti kuendeleza mamlaka nikapewa

ya kuwaza kwa niaba ya jamii.

Hawa wanifuatao wananicha kwa kuweza

kuvyaza mikakati

ya kukabiliana na ulitima walonipagaza kwa ndoto zangu za ujana kuzima.

a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi. **(alama 1)**

b) Kwa kurejelea kifungu hiki taja sababu tatu kwa jibu lako**. (alama 3)**

c) Bainisha vipengele viwili vya kimtindo katika kifungu hiki. **(alama 2)**

d) Eleza sifa sita bainifu za kipera hiki. **(alama 6)**

e) Kipera hiki kinaendelea kudidimia katika jamii yako. Eleza hoja nne utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga hali hii. **(alama 4)**

f) Fafanua umuhimu wa kipera hiki katika jamii. **(alama 4)**

0746 222 000

18. S***oma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*** Malaika nakupenda Malaika Malaika nakupenda Malaika

Nami nifanyeje? Kijana mwenzio

Nashindwa na mali sina we! Ningekuoa Malaika

Pesa zasumbua moyo wangu Pesa zasumbua moyo wangu Nami nifanyeje?

Kijana mwenzio

Nashindwa na mali sina wee Ningekuoa Malaika

a) Tambua utungo huu. **(alama 1)**

b) Thibitisha jibu la (a) . **(alama 2)**

c) Tambua nafsineni katika utungo huu. **(alama 1)**

d) Eleza toni inayojitokeza katika utungo huu. **(alama 2)**

e) Umealikwa kuwasilisha utungo huu mbele ya wanafunzi wa shule yako.Taja mambo sita utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji huu. **(alama 6)**

f) Tambua na uthibitishe shughuli mbili za kijamii zinazojitokeza katika utungo. **(alama 2)**

g) Taja mbinu **mbili** za kimtindo zilizotumika katika utungo. **(alama 2)**

h) Eleza dhima ya utungo wa aina hii katika jamii. **(alama 4)**

19. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata***.

Mabibi na mabwana, ndugu na marafiki hamjambo! Nimefika hapa leo kushuhudia sherehe za vijana hao wanaofuzu kuingia utu uzimani. Tangu jadi mababu zetu waliandaa sherehe kama hizi ili kuwaandaa vijana wao kukabiliana na maisha ya usoni. Wanangu, utu uzima hautokani tu na viviga au kisu cha ngariba. Ni matendo na tabia. Naam, ni matendo na tabia. Katika jamii ya sasa watu humpima mtu kutokana na ufanifu wake kiuchumi, kielimu na kijamii. Mtu asiye na mali yake hubezwa kwa kutofanya bidii inavyostahili. Hivyo basi, nawashauri vijana wanaofuzu leo kuwa, mnafaa kutia bidii masomoni ili mustakabali wenu uwe mzuri. Katika nyakati zetu, ubingwa wetu ulipimwa katika fani ya vita na ngoma. Ungewasikia wanaume wakijisifu kwa wimbo wakisema:

Ooh ooh ooh!

0746 222 000

Mimi ni chuma inayoishi

Ningiapo vitani, macho yangu tu huwafisha wengi. Viganja vyangu vimeiletea jamii yetu fahari Wananiita Ngao.

Juzi ngomani niliwapiku wote

Wanawali waliniangukia kwa kutaka uchumba Nani mwingine kama Ngao?

Hata hivyo, hali katika jamii ya sasa ni tofauti. Ngoma imekuwa nyenzo ya burudani tu. Navyo vita vya kikabila vimepitwa na wakati. Wanaopigana aghalabu huchukiliwa hatua kali za kisheria. Elimu ni silaha ya pekee. Elimu itawafungulia milango ya heri. Ndugu na marafiki, nawaomba nyote muwasisitizie vijana hao umuhimu wa kuwatii walimu wao na kutia bidii masomoni watakaporudi shuleni. Msisite kuwaadhibu wanapokosea. Ni muhimu kukumbuka kuwa, mchelea mwana kulia hulia mwenyewe. Tulisimuliwa na bibi kuwa, hapo zamani za kale mwanamke fulani alificha mnyama hatari aliyekuwa akifukuzwa na mashujaa wa jamii. Baada ya mashujaa hao kuondoka, mnyama huyo alimla mwanamke huyo. Ingawa ni hadithi, kisa hicho kinatufunzwa kuwa, hatufai kuficha matendo mabaya ya wanetu. Tuwarekebishe mapema.

Nikimaliza naomba kuwajuza vijana hawa kuwa, tohara siyo ufunguo wa ulevi. Inahuzunisha kuwakuta vijana wadogo wamelala matopeni kwa kushindwa kutembea kutokana na ulevi. Wengine hubaki pale hadi asubuhi wakitumbuizwa na milio ya vyura. Nina matumaini kuwa, kundi hili litakuwa tofauti. Asanteni kwa kunisikiliza.

a) Tambua kipera katika dondoo. **(alama 1)**

b) Eleza sifa za kipera ulichotaja katika (i) **(alama 4)**

c) Eleza dhima zozote mbili za kipera ulichotaja katika (i) **(alama 2)**

d) Tanzu za fasihi huingiliana na kutegemeana. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu hiki. **(alama 5)**

e) Eleza toni iliyobainika katika kifungu. **(alama 2)**

f) Fafanua mbinu za kimtindo zinazodhihirika katika kifungu hiki. **(alama 6)**

0746 222 000

20. Soma kifungu kifutacho kisha ujibu maswali yanayofata.

Basi kizito Matukio alipewa Cheo kikubwa kutokana na uchapakazi wake. Shirika alilokuwa akifanya kazi likawa na matumaini makubwa. Kizito naye badala ya kuchapa kazi akawa anajigamba na kujitapa mitaani. "Ukubwa ninaujua miye. Mimi ndiye Kizito hapa. Kizito Mzito mimi, akaringa. Akawadharau akina Wanjiku. Amina na Shikuku.

Akajitosa kwenye raha bila kujali na kuvaa suti nzito alizoagizia kwa fedha za shirika. Muda si muda shirika likaingia hasara. Mwishowe ametimuliwa kazini na wazito wenyewe. Ameondoka na mkoba mzito wa madeni na fedheha: nguo sasa anavaa za matambara mazito! Jamani uzito unakowapeleka wazito.

i) Onyesha kwa nini kipera hiki ni soga **(al.4)**

ii) Fafanua vipengele viwili vya kimtindo vilivyotumika katika utungo huu. **(al.2)**

iii) Eleza matatizo utakayokumbana nayo nyanjani ukikusanya kazi ya kipera hiki **(al.4)**

iv) Taja mifano mitatu ya ngomezi za kisasa **(al.3)**

v) Eleza hasara nne za miviga? **(al.4)**

vi) Fafanua umuhimu wa misimu ya kisasa. **(al.3)**

21. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.

Umeanguka mwamba Jabali tuloegemea Lilotupa kimbilio Mahasidi kutishia Mti mkuu umegwa Wana wa ndege wa wapi? Bila shaka hangaiko Metukumba makinda.

Angalikuwa pamwe nasi Maulana mungu wetu Swali hilo tungemuuliza Mbona kaacha mauko Ngome yetu kuvamia? Ela mwenyewe Mwenza Ajua hatima yetu Lilobaki kumwamini Riziki kutuangushia.

<u>Maswali</u>

a) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha. Alama 4

b) Bainisha vipengele vitano vya kimtindo vilivyotumika katika wimbo huu. Alama 5

c) Tungo za aina hii zinaendelea kupoteza umaarufu katika jamii yako. Fafanua hoja nne utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga dhidi ya hali hii. Alama 4

d) Eleza sababu tatu za kukusanya habari kuhusu kipera hiki kwa kutumia mbinu ya kushiriki. Alama 3

0746 222 000

22. Ainisha kifungu kifuatacho cha sifo. Thibitisha kwa hoja nne. Alama 4

Ndimi Kiluki jogoo la kijijini

Jogoo la kijijini liwikialo jijini Jogoo liloyavunja makoo ya jijini Makoo yote yanisifia

Wangu ukoo ni wa wafalme Kilimo ndo nguzo yetu

Kiluki nalima maekari kwa maekari Siku chache natumia

Kandanda nasakata Asonijua Makinduni ni nani? Mbeleni ajitambulishe.

23. ***Soma utungo ufatao kisha ujibu maswali***

"Hapo zamani za kale, kale sana kabla ya ujio wa manabii Issa, Musa ama hata Yesu, walimwengu wote waliishi pamoja kama ndugu na dada. Hakukuwepo haya makabila tunayoyasikia yakitajwa kila siku. Hakukuwepo na utabaka. Hapakuwepo na maskini. Watu wote waliishi pamoja kama wafanyavyo wanyama wa familia moja. Hakukuwepo na tofauti na tamaa ya uongozi na kujitakia kwa wananchi. Ubinafsi.

Mwanadamu alipogundua umoja aliopewa na Mungu wake, alianza kusoma mengi mno na kutaka kujua mengi kuhusu Mola. Alidhani kwamba Mungu aliishi mbinguni. Hivyo basi, wanadamu wote waliitana pamoja katika kamkunji; mkutano wa siri, waratibu jinsi wangeweza kumfikia mwenyezi Mungu. Mwisho wa kikao, walikubaliana kuwa waanze kujenga ukuta mkubwa ambao ungewawezesha kufika juu mbinguni na kuzungumza moja kwa moja na Mola Mkuu.

Siku iliyofuatia waliingia katika kazi. Huyu alileta jiwe hili na huyu msumari huu. Kazi ilifanywa kwa kujitolea na jitihada kuu kila mmoja akiamini kuwa atakaye kilicho mvunguni ni sharti ainame. Aidha, mgaagaa na upwa hali wali mkavu. Ukuta wao ulipanda kwa kasi. Wazee wenye busara walijaribu kuwaonya wajenzi dhidi ya hatua hii yao ila wakashikilia msimamo wao wa kutaka kuonana na Muumba wa mbingu na ardhi ana kwa ana.

Mungu alipoona kuwa mwanadamu amejawa na kiburi, aliwachanganya wajenzi kwa kuzichanganya lugha zao. Hili liliwanya kutoelewana kiasi kwamba fundi mmoja alipoomba aletewa bisibisi aliletewa nyundo. Hatimaye ukuta mzima ulianguka na kuwaangamiza wajenzi na waliosalia wakabaki kutoelewana lugha zao. Hii ndiyo sababu wanadamu wana lugha tofauti."

Kutoka: Meja S. Bukachi- Mola Mkuu (Riwaya)

0746 222 000

a) Tambua kipera hiki cha hadithi. **(Alama 2)**

b) Wewe ni mtafiti uliye nyanjani kwa uchunguzi zaidi kuhusu kipera hiki:

(i) Taja mbinu tatu utakazotumia katika utafiti wako. **(Alama 3)**

(ii) Upi umuhimu wa kukusanya na kuhifadi tungo kama hizi? **(alama 5)**

(iii) Taja njia tano zinazotumiwa na jamii ya kisasa kuendeleza fasihi simulizi. **(alama 5)**

24. Soma makala yafwatayo kisha ujibu maswali yafwatayo

Hapo zamani za kale, paloindokea mtu mmoja kwa jina mzee Kata. Mzee Kata alikuwa na wake wawili. Mke wa kwanza aliitwa Neema na wa pili aliitwa Nduli. Kila mmoja wa wake hawa alikuwa na mtoto mmoja. Neema alikuwa na mtoto wa kike kwa jina Majaliwa.

Majaliwa alikuwa ameumbwa akaumbika.Uso wake ulihimili macho meupe mfano wa theluji. Meno yake ya juu yalipangika kwa njia ambayo iliyafanya kuacha mwanya ambao ulifanya tabasamu yake kuwa ya mvuto wa sumaki. Urembo wa Majaliwa, kama walivyosema wengi, ungemtoa nyoka yeyote pangoni.

Kwa upande mwingine Kutu, bintiye Nduli, alikuwa mwenye sura mbaya ya kutisha.Uso wake usiopendeza ulimfanya kuonekana kama ajuza wa miaka mia moja! Tabia yake ya ukorofi ilikoleza mvuto wake hasi. Vijana wa kijijini walimfanyia inadi kila mara kwa kumkumbusha kuwa hakufaa kuringa. “Sura kama kiboko”, wangemtania

Tofauti za kiumbo kati ya Majaliwa na Kutu zilizua uhasama mkubwa kati ya ndugu hawa, sikwambii mama zao. Hali hii ilizidishwa Zaidi na nongwa za kila siku zilizotokana na ukewenza. Familia yam zee Kata ikawa medaniya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Hali ya mtafaruku iliendelea kuikosesha nyumba yam zee kata amani. Asubuhi moja, Mzee Kata aliamka kama kawaida yake, alijikohoza kama isharaya kutangaza kufika kwake. Daima hakupenda kuzungumza na wakeze asubuhi na mapema. Aliamini kuwa wangemletea nuksi. Kinyume na siku nyingine, mzee Kata hakuitikiwa. Ilibidi kujikaribisha nyumbani mwake.

Mara tu alipovuka kizingiti cha kijumba hicho, alitupa macho yake juu yakitanda cha mayoweambapo mke wake alijinyosha twaa kakauka kama ukuni; hanapumzi. Weupe wa macho yake na mapovu yaliyomtoka kinywani yalimhakikishia Mzee Kata kuwa Neema kampungia mkono. Harufu kali ya sumu ilihanikiza hewa kumwarifu kuwa Mzee kata kuwa mkewe kafa kwa kutendwa na mkemwenza

0746 222 000

Maisha ya Majaliwa yalichukua mkondo mpya baada ya tanzia hii. Mama wa kambo sasa alipata mwanya wa kumhini majaliwa. Kazi zote za nyumbani aliachiwa yeye.Huku Kutu akiachwa huru kucheza. Majaliwa alipewa chakula hapa; wengine wakila biriani yeye alipewa wali wa kawaida. Mavazi yake yaligeuka matambara.Siku zilivyozidi kusonga ndivyo mateso yalivyoongezeka. Mama wa kambo alizidisha wivu wake kwa majaliwa. Hata Majaliwa alipovunja ungo na wachumba kuja kumposa, mama wa kambo aliwafukuzia mbali. Wenine walihimizwa kumposa Kutu. Wachumba waliochachawa kutaka kumuoa majaliwa wakidai kuwa hawamtaki Kutu kwa sababu ya kiburi chake, walinyeshewa matusi, wakahizinika na kujiendea zao.

Siku moja alitokea kijana mmoja makini .alikuja amavalia gwanda jeusi lililojiinamia kwa uchovu. Viatu alivyovaa vilikuwa vimejichokea kwa kupiga lami. Kofia iliokuwa kichwani pake ilitosha kumhakikishia mama wa kambo kuwa huyu alikuwa fakiri. Mama mtu alikubali mara moja posa ya kijana huyu kwa Majaliwa akijua kuwa angeadhibika. Aliamini amemtokomeza Majaliwa ndani ya lindi la ulitima. Mzee Kata naye hakusita kumwoza Majaliwa kwa kiajana huyu maana aliiona hii kama fursa ya pekee ya kumwepusha vitimbi vya mama wa kambo

Majaliwa aliandamana na mume wake hadi Kijiji cha peponi ambako kijana huyu allishi. Wallingia katika nyumba ya msonge ambamo Majaliwa alitarajia kuanza Maisha ya ndoa. Walitayarisha chajio, wakala na kulala.

Asubuhi, Majaliwa aliamshwa na nyimbo za ndege. Alipofunguamacho, alijikuta kalala ndani mya chumba chenye sakafu ya vigae. Ukuta wa chumba hicho ulikuwa wa rangi wa zari.

Mapambo ya dhahabu yalitundkwa ukutani. Kumbe kijana aliyemuoa hakuwa maskini kama ilivyodhaniwa! Alikuwa mwana wa mfalme! Na hili lilikuwa kasri hasa! Majaliwa hakueza kuamini! Alikuwa ameamkia Maisha ambayo hakuwahi yawazia.

Alipoingia sebuleni alimpata mama yake mpenzi, akiwa na tabasamu ya milele usoni. Walikumbatiana kwa shauku kuu. Kumbe kijana huyo alikuwa ametumwa na mamake Majaliwa! Mumewe majaliwa alishuhudia kwa umbali. Machozi ya mama mtu na mwanawe yakilovya vifua vyao na kuyeyusha simanzi na kuyeyusha simanzi iliyokuwa imeyaandama Maisha yao. Tangu siku hiyi, watu hawa wallishi kwa raha mstarehe. Hadithi yangu inaishia hapo.

a) Taja na utolee mifano mbinu sita za kimtindo zilizotumiwa katika utungo huu **(al.3)**

b) Utungo huu unaweza kuainishwa kama ngamo, toa sababu **(al.1)**

0746 222 000

c) Fafanua umuhimu nne wa formula ya kumalizia katika utungo huu **(al. 4)**

d) Taja shughuli moja ya kijamii katika jamii ya utungo huu **(al. 1)**

e) Jadili tatizo moja la ukewenza katika utungo huu **(al.1)**

f) Taja na ufafanue dhima tano ya utungo huu katika jamii yake **(al.5)**

g) Taja mambo mawili ambayo fanani anaweza kutekeleza ili kuufanya utungo huu uwe wa kuvutia Zaidi **(al. 1)**

h) Miviga ni nini? **(al.1)**

i) Taja hasara tatu za miviga **(al.3)**

25. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*** Ndimi Nguli, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma Ndimi dume liloingia nyanjani Makoo yakatetemeka
Yakang'ang'ania gozi kusakata nami.

(a) Tambulisha kipera kinachojitokeza katika kifungu hiki. **(alama 2)**

(b) Eleza sifa tano bainifu za kipera hiki katika fasihi simulizi. **(alama 10)**

(c) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. **(alama 8)**

26. Hamkuona jinsi tulivyowapiga magoli Hamkuona vile tuliwala chenga kila mara
Itakuwaje timu mbovu kama hii Kuchezea miamba kama sisi
Niliwafunga baada ya sekunde wakati ule nitashindwaje leo?

Maswali

(a) Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanue (alama 2)

(b) Fafanua umuhimu wa kipera cha fasihi ulichotambua katika (a) (alama 3)

(c) Fafanua sifa zozote nne za kipera ulichokitaja katika swali la (a) (alama 4)

(d) Ni changamoto zipi zinazoweza kumkumba mtafiti akifanya utafiti wa soga nyanjani (alama 3)

(e) Wewe ni mwigizaji wa michezo ya jukwaani. Eleza mambo sita ambayo utazingatia ili kufanikisha uigizaji wako.
(alama4)

(f) Onyesha jinsi methali ni utanzu tegemezi kwa kueleza miktadha ambapo hutumiwa.**(alama 4)**

0746 222 000

27. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

(a) A: Kumbe mambo yenyewe rahisi hivi?

B: Rahisi, lakini usije ukabakwa tena

A: Hapana, safari hii itakuwa zamu yako. *(Alimrudishia … huku akichekacheka)*

C: Hapajaharibika mambo mama'ngu. Kwani la ajabu lipi? Sasa miye namsubiri Bakari mpya tu, hichi kikongwe nikipe talaka.*(Akitabasamu)*

D: Haachwi mtu hapa. Tutabanana humo humo. Yeye atakuwa mke mdogo na mimi mkubwa.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. **(alama 1)**

(ii) Toa sababu **mbili** kuthibitisha jibu lako la (i) hapo juu. **(alama 2)**

(iii) Eleza manufaa saba ambayo jamii hunufaika nayo kwa kushiriki katika kipera **hiki.** **(alama 7)**

(b) ***Soma kifungu ufuatao kisha ujibu maswali.***

Siwezi kuhututubu. Mimi sikuwafundisha ubaguzi. Kwa nini mnabaguana? Kwa nini hamukuwapa watu wa matabaka yote nafasi ya kuzungumza? Kwa nini? Kwa nini mnafanya hali hii ya kuwa kuna watu na nusu watu? Nataka wazungumze wale ambao hawata sifu tu.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. **(alama 2)**

(ii) Eleza mitindo mitatu katika kifungu hiki. **(alama 3)**

(iii) Eleza majukumu matano ya kipera hiki katika jamii. **(alama 5)**

28. ***Soma utungo ufatao kisha ujibu maswali***

Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu, Nami ndiye niliompa uhai mwana unoringia, Anokufanya upite ukinitemea mate,

Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika, Miungu na waone chozi langu, wasikie kilio changu, Mizimu na waone uchungu wangu,

Radhi zao wasiwahi kukupa, Laana wakumiminie,

Uje kulizwa mara mia na wanao,

Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao, Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha, Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!

(Kutoka: Assumpta K. Matei- Fani ya Fasihi Simulizi, uk 145)

(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi **(alama 2)**

(b) Jinsia ya nafsi neni ni gani? **(alama 2)**

0746 222 000

(c) Eleza sifa zozote sita za kipera hiki cha fasihi simulizi. **(alama 6)**

(d) Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii. **(alama 4)**

(e) Fafanua njia sita jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi**.(alama 6)**

0746 222 000

Ukihitaji majibu,

Pigia bw. Isaboke

0746 222 000

MWISHO

0746 222 000

SET BOOKS AVAILABLE WITH US

- ✓ *Artist Of The Floating World*
- ✓ *Bembea Ya Maisha*
- ✓ *Mapambazuko Ya Machweo*
- ✓ *Nguu Za Jadi*
- ✓ *Fathers Of Nations*
- ✓ *Silent Songs And Other Stories*
- ✓ *A Parliament Of Owls*
- ✓ *The Samaritan*

0746 222 000

OTHER SETBOOKS GUIDES AVAILABLE				
SETBOOK	**GUIDE**	**QUESTIONS & ANSWERS**	**VIDEOS**	**CONTACT**
Bembea Ya Maisha	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Mapambazuko Ya Machweo	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Nguu Za Jadi	✓	✓	✓	*0746-222-000*
	ENGLISH SETBOOKS			
Fathers Of Nations	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Silent Songs And Other Stories	✓	✓	✓	*0746-222-000*
A Parliament Of Owls	✓	✓	✓	*0746-222-000*
The Samaritan	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Artist Of The Floating World	✓	✓	✓	*0746-222-000*

0746 222 000

FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS

0746 222 000

CALL/TEXT/WHATSAPP

0746 222 000

OR

0742 999 000

0746 222 000

mwalimuconsultancy@gmail.com

This is a Product of Mwalimu Consultancy Ltd.

0746 222 000

Powered by Mr Isaboke

0746 222 000

SUCCESS

0746 222 000

REGARDS

0746 222 000

0746 222 000